# *MFALME ALIYEKATALIWA*

. . . kusudi utukufu wa Mungu uletwe juu yetu leo kwa njia ya kuhudumiwa kwa Neno. Na ni . . . Juma hili lililopita nimekuwa kwa namna fulani kidogo nimewezwa na hali ya hewa—siyo kusema hasa kuwezwa na hali ya hewa; ilikuwa ni uchunguzi ulionilazimu kufanyiwa, uchunguzi wa mwili; na hiyo ndiyo sababu mlisikia nilikuwa hospitalini. Sababu yake ilikuwa ni kwamba isinibidi kurudi na kwenda kuvuka mto. Unafanyiwa uchunguzi wa upande wa juu wa tumbo na upande wa chini wa tumbo nao inawabidi ku-. . . kila baada ya dakika chache inawabidi kuja na kukupiga picha tena.

Bali inatupasa kufanyiwa uchunguzi (iwapo sisi hufanya safari za umishenari nchi za ng'ambo) kila miezi sita. Ndugu Roberts na hao wengine, nafikiri, wanafanyiwa wao kila baada ya miezi sita, bali mimi sikuwa nimefanyiwa uchunguzi kwa muda wa miaka minne.

Shida—mimi kweli siyapendi hayo mafuta ya mbarika. Hilo ndilo jambo pekee. Nao wanasema hakuna kitu kingine wanachoweza kumpa mtu badala yake, kwa hiyo mimi . . . Loo, niliumwa sana waliponipa kitu hicho. Mwajua, nimewasimulieni katika hadithi ya maisha yangu jinsi kitu hicho hunifanya niwe mgonjwa sana, nami nachukia tu kunywa kitu hicho. Nami nilimwambia rafiki yangu daktari mwenye fadhili, "Kama kuna . . . je! hamna kitu kingine?"

Yeye akasema, "Sidhani, Ndugu Branham."

Loo, wakati yule bibi alipoingia pale na—kilionekana kama—labda ninatia chumvi, bali kilionekana kama kisaga. Sijaona mengi namna hiyo; nami ningeshikilia pua langu na kuziba kinywa, bali hatimaye niliyameza.

Bali sasa, katika majaribio yote na yote niliyopitia, nataka kumshukuru Bwana kwa uchunguzi mkamilifu. Nami nilipita asilimia mia moja; naweza kwenda po pote ulimwenguni ninakotaka kwenda. Niliwauliza hao madaktari, ambao walikuwa ni watatu wa wataalamu walio bora sana, nafikiri, katika Louisville, nami nikawauliza, nikasema, "Mimi nina udhaifu wa asilimia kumi kwa vyo vyote vile?"

Yeye akasema, "Wewe huna hata chembe moja ya udhaifu." Akasema, "Wewe una afya nzuri sana kwa kila hali." Nami ninamshukuru Mungu sana. Ingetoka kwa nani mwingine ila Baba yetu wa Mbinguni, mnaona, kuwa namna hiyo. Kisha akasema, "Mtiririko wako wote unaonyesha mle ndani ya kwamba ungekuwa kijana." Akasema, "Chembechembe zako za damu hata hazijaanza kuvunjika ama cho chote kile." Akasema, "Uko katika hali nzuri sana, Ndugu Branham."

Ndipo nikasema, "Vema, ninashukuru sana."

Nami nilijaliwa kuzungumza, kumshuhudia kila nesi katika hospitali ile na kila daktari kwa Ufalme wa Mungu. Na daktari fulani mmoja—nafikiri anapaswa kuwa hapa asubuhi ya leo. Nami nina furaha kujua ya kwamba kungali kuna watu wazuri duniani humu—watu halisi. Watu ambao wangenifanyia uchunguzi wa mwili kwa siku tano, ambao labda ungegharimu labda dola mia mbili ama mia tatu kwa kila mmoja; nilipomaliza, walisema, "Ni matoleo yetu kwa ajili ya kazi ya Bwana ambayo unafanya." Si hata . . . Kasema, "Mbona, unatutahayarisha kwa kutuuliza kama tunakuwia sisi." Kasema, "Maombi yako tu kwa ajili yetu sisi."

"Na mle ndani," wao wakasema, "tunaona hangaiko la namna fulani ambalo hatuwezi kufahamu." Kisha kasema, "Haionekani kama kwamba . . . " Akasema, "Kwa nje, wewe huna wasiwasi wala husumbuki, ila" kasema, "mle ndani, kuna hangaiko tusiloweza kufahamu."

Nikasema, "Kama mtaketi hapa kwa muda kidogo tu, nitawaambia." Nami nikaingilia kuzungumza juu ya maono. Ilikuwa fani nyingine kwao. Hawakujua kitu kuhusu jambo hilo. Nikawaambia juu ya Biblia. Kisha nikawaambia juu ya ono alilonipa Bwana hivi majuzi, nao wakalia kama watoto wachanga—waliketi tu pale na kulia.

Kisha nikasema, "Natumaini ya kwamba ninyi hamnifikirii kuwa mshupavu fulani wa dini mwenye kichaa ama baadhi ya . . . "

Kasema, "Hasha, Ndugu Branham. Ninaamini jambo hilo kwa moyo wangu wote." Akasema, "Ila tu nataka kusema jambo moja, huendi shuleni kusomea mambo hayo;" kasema, "ninaamini ya kwamba hayo hutoka kwa Mwenyezi Mungu." Na hao walikuwa watatu wa madaktari wanaojulikana sana katika Louisville, ndio walio bora sana waliokuwa nao. Na kwa hiyo, nilifurahia jambo hilo sana na kujua ya kwamba labda Bwana aliniacha nipande mbegu chache kule.

Kila nesi, nilizungumza nao . . . Asubuhi moja, nilipokuwa nikitoka kwenye chumba cha kupigia picha, nilimwambia yule . . . nilimwangalia maskini mwanamke kizee; alikuwa mgonjwa sana. Nami nikaendelea kushuka chini, kushuka chini, hata nikamfikia. Nilifikiri labda yuafa, nami nikasema, "Nataka kukuuliza swali, dada."

Akasema, "Naam, bwana?"

Nikasema, "Wewe ni Mkristo?"

Naye akasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa fulani."

Basi nikasema, "Nataka kufafanua jambo hilo kidogo," nikasema, "Na—nataka kujua kama wewe ni Mkristo, Mkristo halisi. Ili kwamba kama ungevuka bahari hii ya maisha uingie

kwenye ile nchi nyingine, je! unampenda Yeye?" Nikasema, "Kweli ungeokolewa?"

Naye akasema, "Naam, bwana, ningeokolewa."

Basi nikasema, "Mungu aubariki moyo wako basi. Haidhuru upepo utavuma upande gani, wewe uko salama basi. Mradi tu ndivyo mambo yalivyo." Na kama tu tutatembea kila mahali, bado kungali kuna watu wengi sana wazuri waliosalia ulimwenguni.

Sasa, leo nimekuja na ono ambalo nitawaambia baadaye kidogo, na ningetaka kuzungumza kwanza juu ya baadhi ya Neno kwa maana ninaamini ya kwamba Neno ni muhimu sana—ndilo lililo muhimu sana sasa.

Naam, ninafurahi kumwona Charlie Cox na Ndugu—marafiki wangu wanaosimama pale pamoja—Ndugu . . . siwezi kukumbuka . . . Jefferies (siwezi kulikumbuka jina lake), wengi wenu ninyi ndugu wengine wa thamani kutoka Georgia, kutoka mahali mbalimbali nchini—rafiki msiri wangu wa kale, Bill, anayeketi hapa (naamini ndiye) asubuhi hii, na—na wengi . . . ndugu kutoka Georgia pale, watu walionipa suti hii. Mwajua, hiyo ndiyo moja ya suti zuri sana nilizowahi kuvaa. Ninajisikia vizuri sana. Kweli ni zuri sana na . . . Nawathamini sana. Nitakapowaambia yaliyotendeka katika siku hizi chache zilizopita, mtaona kwa nini ninafikiri ninathamini jambo hilo sana.

Naam, naamini kama ni mapenzi ya Bwana, ninataka kupiga vita sana kuliko hapo awali maishani mwangu, kwa maana ninaona sasa kama—bila shaka, ningeweza kufa leo. Hiyo ni- . . . hamjui. Mtambo wa stima wa kupima moyo na kila kitu, picha kumi na sita mbalimbali—uchunguzi mkamilifu wa mwili ulionyesha ya kwamba nilikuwa mzima kama mtu ye yote angeweza kuwa—mwanadamu duniani. Kwa hiyo ninashukuru kwa jambo hilo. Bali mambo yote, hata hayo yote, na hata ingawa ninamshukuru na kumtolea Mungu shukrani kwa maana mimi ninaamini kwamba Yeye yungali ananiweka katika huduma Yake, haikuwa vile alivyonionyesha mimi muda kidogo tu kabla ya hayo, mnaona. Jambo hilo lilinifurahisha sana.

Sasa, nafikiri usiku wa leo . . . Ni sawa kwako? [Ndugu Neville anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Ndugu ye—yetu mpendwa ni mtu mmoja asiye mchoyo, ndivyo alivyo Ndugu Neville. Na kama ye yote wenu alikuwa hapa Jumapili iliyopita na kuusikia ule ujumbe mzuri sana aliouleta juu ya, *Ile Chupa ya Mafuta*—ulikuwa mmoja wa jumbe nzuri sana nilizowahi kusikia, ulikuwa ndio aliouleta Ndugu Neville kwa Roho Mtakatifu Jumapili iliyopita kwa ajili ya kundi hili dogo la kondoo ambalo Mungu amekusanya pamoja. Na kama ni vema, inampendeza Bwana, na pia Ndugu Neville na kanisa, nataka kuzungumza tena usiku wa leo, nianze mfululizo wa

masomo ya tuseme Jumatatu usiku, namaanisha Jumapili usiku, na Jumatano usiku na Jumapili ijayo—mfululizo wa yale niliyosoma . . .

Isingenilazimu kukaa kule hospitalini bali wao walikuwa wema sana kwangu. Walinipa hicho chumba kwa theluthi moja ya gharama yake, na kwa hiyo nilichukua tu Biblia zangu, vitabu vyangu, na kujitegemeza kitandani, ndipo nikaketi "kitako" pale na kuzileta Biblia zangu zote na kadhalika karibu, na kwa kweli nilikuwa na wakati mzuri—hadi walipoyaleta hayo mafuta ya mbarika. Wakati wangu mzuri ukakoma pale pale; nilikuwa nimekwisha basi. Lakini, Ndugu Pat, nilikuwa mgonjwa kweli. Kitu hicho kweli siwezi kukivumilia. Bali nilikuwa na wakati mzuri kule siku tatu au nne za kwanza.

Nilikuwa na wakati mzuri, nami nilikuwa nikisoma Kitabu cha Waefeso. Loo, huko kukaa pamoja kwa Kanisa, nami nafikiri ni jambo nzuri.

Na—na endapo una kanisa unalohudhuria, wewe nenda moja kwa moja na ushikilie wajibu wako, bali endapo huna kanisa, nawe ungetaka kuja usiku wa leo, na Jumatano usiku, na Jumapili usiku, ningetaka kuchukua usiku wa leo, Kitabu cha 1 cha Efeso, na Jumatano usiku sura ya 2 ya Waefeso, na Jumapili ijayo, sura 3 ya Efeso kuliweka kanisa katika utaratibu. Mnajua ninayomaanisha—ni kuliweka, mahali pake, nami nafikiri ni kulijenga kanisa.

Naam, mimi si- . . . Ninalizungumzia hili wanaohudhuria Maskani ya Branham. Na kama mmoja wenu enyi ndugu wapendwa . . . najua wengine wenu, nafikiri, wana mikutano. Ndugu zetu kule Sellersburg na wengine wana mikutano. Sasa tazama, hiyo ni mikutano ya ufufuo. Ihudhurieni hiyo. Wao ni watumishi wa Kristo—vijana ambao wanasimama katika pengo ambao wametoka. Wakati hata makanisa yao wenyewe yalikataa Ukweli na mambo kama hayo, waliondoka wakaliacha moja kwa moja, ndipo Mungu akawaita katika huduma.

Naam, bwana, na—namheshimu mtu . . . hata siwezi kulikumbuka jina la mtu huyo. Bali yeye ni jamaa mdogo; mzuri, jamaa mwenye sura nzuri na mke mzuri na watoto.

Na—na Ndugu Junie Jackson amekuwa na mikutano michache hapa chini, ambaye ni kumbukumbu nyingine ya ajabu ya neema ya ajabu ya Mungu.

Na wakati wanapokuwa na ufufuo katika makanisa yenu, ninyi ihudhurieni kwa maana hiyo ni ninino yenu—hilo ndilo jambo la kufanya kwa sababu hujui—huenda ikawa mwenye dhambi atakuja madhabahuni, nawe unaweza kushawishiwa kumleta mtu huyo kwa Kristo, jambo ambalo litakuwa dhawabu yako kuu huko ng'ambo. Huku ni kufundisha tu na kuliweka kanisa katika utaratibu hapa kwenye Maskani, tukisaidia tunaposonga mbele.

Sasa, sikuleta saa yangu, kwa hiyo itambidi mtu fulani kuniangalilia. Doc tayari amenionyesha ya kwamba anayo, kwa hiyo ndugu yangu. . . [Ndugu Branham anazungumza na ndugu yake, Edgar "Doc" Branham—Mh.]

Naam, sitazungumza kwa muda mrefu sana. Sasa, iwapo kuna wageni kwenye malango yetu, bila shaka tunataka kuwakaribisha kwa mioyo yetu yote. Mnakaribishwa sana katika maskani haya madogo. Hatuna jengo zuri sana. Tuna mradi wa kujijengea, si mahali pakubwa, bali tu. . . Hili limechakaa sana, nasi tutajaribu kujijengea kanisa dogo na la kupendeza hapa mara tu Bwana atakapotujalia kufanya hivyo. Na wengi wenu wanajitahidi kufanya jambo hili, nasi bila shaka tunafurahia jambo hilo.

Sasa, nataka mfungue pamoja nami, asubuhi hii, katika kusoma I Samweli sura ya 8 na tuanzie manamo—hebu tuanzie mnamo aya ya 19, aya ya 19 na 20, labda, tupate fungu dogo kwa ajili ya somo letu. Na sasa mnapofungua, na kabla. . . Sisi, kile. . . Tutalisoma, halafu tunataka kuingia katika maombi; na iwapo kuna haja zo zote asubuhi hii, basi sema, "Nikumbuke tu?"

Katika ninino yetu ya mwisho—majuma mawili yaliyopita, ama matatu, nilipokuwa na ule mkutano. . . Aisee, walakini, wakati mnapofungua, ile mikutano itaanza kule Chautauqua tarehe sita sasa. Tunatarajia wakati mzuri sana—Middletown, Ohio. Ninyi mlio na likizo zinazokuja, njoni—tukiwa na kambi kubwa karibu kabisa na mto mahali ambapo yote—mahubiri yote uliyowahi kusikia. Wote wako kila mahali mtoni—wahubiri kila asubuhi, siku nzima na usiku kucha. Kwa hiyo wote hukusanyika pamoja. Ni eneo kubwa sana la kambi, kubwa sana kuliko Silver Hills—mara nyingi— halafu eneo kubwa pale ambapo tunaweza kuweka kati ya watu elfu nane na elfu kumi, na kila mara pamejaa watu. Tuna nyakati nzuri sana huko Ohio.

Na mzee Ndugu Kidd, ambaye nilienda kumwombea hivi majuzi asubuhi—nyote mnakumbuka nikiwaambia majuma matatu yaliyopita; daktari alimpa masaa ishirini na manne kuishi-yeye ni mzima na anatembea kila mahali. Yeye alinukuu Andiko; wimbo ambao asingeweza kuuimba. Na wakati nilipoingia na kumtazama hivi majuzi asubuhi na ile shali dogo juu yake; (Niliondoka hapa yapata masaa matatu au manne kabla hakujapambazuka kusudi niweze kumpata) kasema yeye angekufa siku hiyo—kansa katika kibofu.

Na mkewe mpendwa alikuwa anafua kwa senti hamsini kwa siku. Na hiyo ni kabla ya mapambazuko mpaka baada ya usiku kwa senti hamsini kumweka mumewe uwanjani kama mhubiri. Alihubiri ufufuo wa majuma mawili, akachukua sadaka, naye akapata senti themanini. Lakini niliwaona wameketi pale hivi majuzi asubuhi—maskini hao mume na mke wazee (ama maskini

mume na mke, hasa) wameketi pale, huku shali yake iko juu ya bega lake; na mmoja wa waongofu wake—umri wa miaka tisini na miwili na yungali mchangamfu na mwangafu na Mpentekoste kwelikweli, naye ameketi pale, mwajua.

Nami nikasema, "Mnajua, kwa nini ninyi wazee mnaketi hapa?"

"Tunangojea mashua ije." Hilo tu.

Kazi yao, yote waliyofanikiwa; wamefanikiwa kupata waliyokusudia, nao wako tayari kwenda wakapate thawabu yao. Nami nikamwambia Ndugu...?...ya kwamba... nikamwambia Ndugu Kiddson...Kidd asubuhi ile, "Utakuwa kwenye ule mkutano wa Chautauqua."

Yeye alinipigia simu jana, kasema, "Nitakuwapo, Ndugu Branham." Ilikuwa sawa tu.

Mingi ya mikutano yangu kutoka kwenye huduma yangu mpya inayokuja. Ndugu fulani—ndugu wa Kibatisti anayesimama hapa—bintiye, tineja, alikuwa kwa namna fulani amepotoka, nami nikamwambia, "Namtoa binti yako kwa Bwana Yesu," asubuhi ya hivi majuzi, na wakati alipoenda nyumbani yeye aliokoka, na yule mwingine yuko hapa asubuhi ya leo kubatizwa, na wanaendelea.

Na mtu fulani, Bw. Sothmann, rafiki yangu kutoka Canada—mama mkwe wake, katika hali ya kufa, kasema, "Utampata mama mkwe wako, utakapofika kule, mzima, akiendelea kupata nafuu na akiwa mzima." Hivyo ndivyo ilivyokuwa tu. Na ninino tu...watu wakiingia tu. Iko katika uchanga wake sasa, ikiendelea. Bali loo, tunatarajia mengi sana, mengi mno juu ya yote. Tuko katika siku mbaya na za mwisho bali katika saa yenye utukufu.

Basi, mmefungua Biblia zenu tupate kusoma?—sura ya 8 ya Samweli. Nami nilimwahidi Gene kukaa pale nyuma kunakorekodiwa, haya yaliyosalia...tulikuwa tu tunaanza katika mkutano wetu.

> *Walakini hao watu wakakataa kuisikiliza sauti ya Samweli; wakasema, Siyo hivyo; lakini tunataka kuwa na mfalme juu yetu;*
>
> *Ili sisi...tufanane na...*taifa, *mataifa yote; tena mfalme wetu atuamue, tena atoke mbele yetu na kutupigia vita vyetu.*
>
> *...Samweli akayasikia maneno* haya *yote ya watu, akayanena masikioni mwa Bwana.*
>
> *Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti yao, ukawafanyie mfalme. Kisha Samweli akawaambia watu wa Israeli, Enendeni kila mtu* kwenye mji *wake.*

Naam, kama ningejaribu kuchagua kutoka hili asubuhi hii kitu ambacho ningekiita somo kwa ajili ya dakika chache zijazo, ningetaka kuchagua somo la: *Mfalme Aliyekataliwa*.

Ulikuwa wakati ambao kama, katika nyakati zote, kwamba watu daima hawakutaka Mungu awaongoze. Wao wanataka njia yao ya uongozi. Na hadithi hii asubuhi ya leo—na mtakapoenda nyumbani kwenu, ingekuwa vizuri kwenu kuisoma yote. Ilikuwa katika wakati wa siku za Samweli, yule mtu wa Mungu—nabii. Naye alikuwa mtu wa haki na mtu mzuri—mwenye heshima, mwenye sifa nzuri, wa kweli, na mtu mwaminifu kwa watu, hakuwadanganya kamwe, na hakuwaambia kitu ila moja kwa moja, "BWANA ASEMA HIVI."

Bali watu walikuwa wamefikia mahali ambapo walikuwa wanataka kubadilisha mpango huu. Walikuwa wamewaangalia Wafilisti na Waamaleki, Waamori, Wahiti, na mataifa mengine ya ulimwengu, nao walikuwa wameona ya kwamba walikuwa na wafalme waliowatawala, wakawaongoza, wakawaelekeza, wakapigia vita vyao, na kadhalika. Na hii ilionekana kana kwamba Israeli walitaka kujifananisha wenyewe na hawa wafalme na watu hawa.

Bali haijakuwa hivyo kamwe, katika kizazi cho chote, mapenzi ya Mungu kwa watu Wake kutenda kama watu wa ulimwengu, ama kuongozwa ama kutawaliwa kama watu wa ulimwengu. Watu wa Mungu daima, wamekuwa, watu wa kipekee, watu tofauti, watu walioitwa watoke, watu waliotenganishwa, watu walio tofauti kabisa katika matendo yao, katika njia zao, katika hali yao ya maisha, na vile watu wa ulimwengu walivyo. Tamaa ya mambo na maumbile yao yalivyo, yamekuwa daima kinyume cha mambo ambayo watu wa ulimwengu wanatamani.

Nao watu wa Israeli wakamjia Samweli wakasema, "Sasa unakuwa mzee, na wanao hawazifuati njia zako;" (kwa sababu hawakuwa waaminifu kama Samweli; walikuwa watu wa kuhonga na kuchukua fedha). Nao wakasema, "Samweli, vijana wako si kama ulivyo wewe, kwa hiyo tunataka utoke uende ukatutafutie mfalme, kisha umpake mafuta, na kutufanya sisi watu kama watu wengine wa ulimwengu."

Ndipo Samweli akajaribu kuwaambia ya kwamba jambo hilo halitafanikiwa. Akasema, "Kama mkifanya hivyo, muda si muda, mtakuta kwamba atawaita wana wenu wote kutoka manyumbani mwenu na kuwafanya askari wa kukimbia mbele ya magari yake na kubeba silaha na mikuki. Isitoshe, bali atawaita binti zenu na kuwafanya waokaji wa mikate na kuwatoa kwenu waende wakalilishe jeshi." Kisha akasema, "Mbali na hayo yote, atawatoza ushuru fulani, wa nafaka yenu, na mapato yenu yote. Yeye atatoza ushuru hivyo vyote apate

kulipa deni fulani za serikali na kadhalika ambazo hazina budi kulipiwa." Akasema, "Nafikiri kwa jumla mnafanya kosa."

Lakini watu waliposema, "Bali tungali tunataka kuwa kama watu wengine."

Kuna kitu fulani katika wanaume na wanawake kwamba wao hutaka kufanana. Na kuna Mtu mmoja tu aliyepata kuishi duniani ambaye alikuwa kielelezo chetu, na huyo alikuwa Yule aliyetufia sisi sote, Bwana na Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Yeye alikuwa mfano mkamilifu wa jinsi inavyotupasa kuwa—daima akifanya kazi ya Babaye na kufanya yaliyo mema.

Na haidhuru jinsi gani Samweli alivyojaribu kuwashawishi watu hao, daima walimfuata usiku na mchana, "Tunataka mfalme. Tunataka mtu. Tunataka mtu tunayeweza kusema, 'Huyu ndiye kiongozi wetu." Na jambo hilo halijawahi kamwe kuwa mapenzi ya Mungu. Haijakuwa kamwe mapenzi ya Mungu, ama haitakuwa kamwe mapenzi ya Mungu mtu kumtawala mwingine. Mungu humtawala mwanadamu. Mungu ndiye Mtawala wetu, Mfalme wetu. Na hilo linaenda sambamba sana, linaenda sambamba sana na siku hizi kwa maana inaonekana mwanadamu ana wazo lile lile. Inaonekana wanashindwa kutambua kwamba Mungu angali anamtawala mwanadamu, badala ya mwanadamu kumtawala mwanadamu.

Kwa hiyo, walijichagulia mtu aliyeitwa Sauli, aliyekuwa mwana wa Kishi. Naye alikuwa mtu mwenye sifa nzuri, mheshimiwa. Bali aliwafaa watu kabisa kwa maana alikuwa mtu mkubwa mno, mrefu, mtu wa tabaka bora. Maandiko yanasema tangu begani kwenda juu hadi kichwani alikuwa mrefu kuliko mtu ye yote katika Israeli. Alionekana kama mfalme, naye alikuwa mzuri wa uso. Alikuwa mtu mwerevu na mtu asiye wa kawaida.

Sasa, huyo ndiye mtu watu wanayetaka kuchagua siku hizi. Inaonekana watu hawaridhiki na vile Mungu alivyoliweka Kanisa Lake litawaliwe na kuongozwa na Roho Mtakatifu. Wanataka mtu fulani, mtu fulani, madhehebu fulani, watu fulani waliongoze kanisa, kwamba wanashindwa kujitupa wenyewe kabisa katika mikono ya Mungu wawe wa kiroho, waongozwe na Roho Mtakatifu. Wao wanataka mtu fulani awafanyie ibada, mtu fulani ambaye atawaambia namna tu ya kufanya mambo na kila kitu. Kwa hiyo ilionekana kwamba mtu huyu anafaa mahali hapo kabisa, kwa maana alikuwa mtu mwenye akili sana.

Na ni kama ilivyo siku hizi kabisa. Sisi tunapenda kuwachagua watu kama hao, pia, kuyaongoza makanisa yetu, kuliongoza Kanisa la Mungu. Mimi sina neno dhidi yake, ila tu ni kusema jambo fulani, ya kwamba siyo, haikuwa hivyo, na haitakuwa kamwe mapenzi ya Mungu kwa jambo hilo kutendeka. Mungu atawatawala watu Wake, kumtawala kila mtu.

Ndipo tunaona ya kwamba huyu mwana wa Kishi—mtu mkuu, na kimo chake, na ninino yake. . . Ilionekana kwamba anawafaa watu na kwamba joho lake juu yake lingeonekana zuri sana na taji kichwani mwake, akiwa juu sana ya watu wengine wote alipotembea, angekuwa tunu hasa kwa ufalme wa Israeli. Kwa maana wafalme wengine wa mataifa mengine wangefikiri, "Angalia jinsi alivyo mtu wa ajabu!" Jinsi wangeelekeza vidole vyao na kusema, "Angalieni hapa jinsi tulivyo na mfalme mkuu! Angalieni ni mtu mkuu jinsi gani anayetutawala!"

Na inasikitisha kusema, bali ni kweli jinsi gani leo kwa kanisa. Wao wanapenda kusema, "Mchungaji wetu si mtu mwenye akili chache; yeye ni mtu mkuu. Yeye amehitimu kutoka Hartford ama shule mashuhuri ya theolojia. Ana digrii nne kutoka mahali *fulani na fulani*, naye ni mtu anayejua kuchanganyikana sana na watu." Hayo yote yanaweza kuwa sawa na yana mahali pake, bali njia ya Mungu kwa Kanisa Lake ni kuongozwa na Roho Mtakatifu na Roho Wake. Bali wao wanapenda kusema kwamba, "Tuna madhehebu haya makubwa mno ambayo sisi ni wafuasi wake. Tumeanza kule nyuma katika siku za mwanzoni wakati tulipokuwa katika uchache, watu wachache tu na wadogo. Na sasa tumestawi hata kufikia mahali ambapo sisi ni miongoni mwa madhehebu makubwa sana yaliyopo. Tuna shule zilizo bora sana na wahudumu walio na elimu sana. Tuna umati uliovalia vizuri sana, na watu wenye elimu sana jijini huhudhuria madhehebu yetu. Nasi tunawasaidia maskini, na tunafanya matendo mema na hayo yote;" na hakuna hata kidogo—Mungu na anizuie nisiseme neno moja dhidi ya jambo hilo, kwa maana hayo yote ni mema; bali hata hivyo si mapenzi ya Mungu kwamba mwanadamu amtawale mwanadamu.

Mungu alituma, kwenye Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu kuitawala mioyo ya wanadamu na kuyatawala maisha yao. Haikukusudiwa kwamba mwanadamu amtawale mwanadamu, bali sisi tunapenda kusema hivyo.

Ni jambo kubwa mno tunapoweza kusema sisi ni washiriki wa shirika kubwa sana: "Wewe ni Mkristo?"— hivyo ndivyo nilivyolipata somo hili. Nilipokuwa hospitalini, na ningemuuliza mtu mmoja, "Wewe ni Mkristo?" "Mimi ni mfuasi wa *fulani na fulani*."

"Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni mfuasi wa *fulani na fulani*." Na maskini yule nesi akaja karibu na kitanda changu ambapo nilikuwa ninasoma Biblia yangu, naye alikuwa nesi mgeni sehemu ile, naye akasema, "U hali gani?" Akasema, "Ninaamini wewe ni Kasisi Branham aliyekuja hapa kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa mwili."

Nikasema, "Naam."

Naye akasema, "Naomba nikusugue mgongoni kusudi ujisikie afadhali kidogo, kwa spiriti?"

Nami nikasema, "Waweza kufanya hivyo?"

Na wakati alipokuwa ananisugua mgongoni, yeye akasema, "Wewe ni mfuasi wa madhehebu gani ya kanisa?"

Nami nikasema, "Loo, mimi ni mfuasi wa madhehebu ya kale sana yaliyopo."

Naye akasema, "Ni madhehebu gani hayo?"

Nikasema, "Ni yale yaliyoundwa kabla ulimwengu haujaundwa."

"Loo," akasema, "nini . . . siamini ninayajua hayo . . . " Akasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa fulani. Ni shirika hilo?"

Nikasema, "La, mama. Hilo liliundwa tu yapata miaka mia mbili iliyopita—shirika hilo. Bali shirika hili lilianza wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha, walipoona kule kuja kwa Mwokozi kuikomboa jamii ya wanadamu."

Naye akaacha tu kuusugua mgongo wangu, nami nilikuwa nimeinama kidogo hivi kusudi bibi huyo apate kusugua, (naye alikuwa anatoka karibu na Corydon hapa chini,) nasi tukaingilia kuzungumza, ndipo akasema, "Bwana, daima nimeamini ya kwamba kama Mungu aliwahi kuwa Mungu, Yeye yuangali Mungu leo kama tu alivyokuwa katika siku za kale." Akasema, "Ingawa kanisa langu hukataa kata kata jambo hilo, bali mimi naamini ya kwamba ni Kweli."

Nami nikasema, "Wewe huko mbali na Ufalme wa Mungu, ewe msichana."

Akasema, "Kama Yeye alipata kuwa Mponya, je! Yeye si angali Mponya?"

Nikasema, "Bila shaka ndivyo alivyo Yeye, dada yangu."

Bali mwanadamu anataka kutawala, na kumtawala mwanadamu; na mwanadamu anataka mwanadamu amtawale. Yeye hataki Mungu atawale.

Kwa hiyo huyu mwana wa Kishi (Sauli, kwa jina) alikuwa tu jibu walilotaka. Yule mtu mkubwa wa kimo naye . . . loo, yeye angewaongoza kweli vitani, na kadhalika. Ila hata hivyo hiyo haikuwa njia ya Mungu ya kutenda mambo. Mungu alitaka yule nabii Wake mzee mwaminifu kuwaongoza na kunena maneno Yake kwao.

Sasa, leo, katika wakati wetu mkuu wa kanisa tunaoishi, sisi—nafikiri na kuamini hili kwa moyo wangu wote ya kwamba tumeenda vinginevyo kabisa kutoka yale Mungu aliyotuagiza kutenda. Maneno ya mwisho ya Mwokozi wetu yalikuwa katika Marko 16, kasema:

> . . .*Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; basi asiyeamini, atahukumiwa.*
>
> *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu* wao *watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*
>
> Na kama wao wangeshika *nyoka;* ama *wakinywa* . . . vitu vya *kufisha* havingewadhuru *kabisa,* na kama *wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa,* . . .*watapata afya.*

Hapana mtu; hamna mwana wa Kishi, ama mtu mwingine ye yote anayeweza kuleta hayo nje ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Bali tumejenga shule; tumejenga seminari, na kufanya mashirika ku—kuridhisha na kuonekana kama walimwengu wengine.

Naam, Roho Mtakatifu alikuwa ndiye kiongozi katika taifa hili. Taifa hili lilikuwa linatawaliwa wakati huko nyuma . . . walipouandika ule Mkataba wa Uhuru, na kulikuweko na kiti cha ziada kimewekwa pale. Hapana shaka moyoni mwangu ila kwamba Mwana wa Mungu aliketi pale mezani. Wakati taifa hili lilipoanzishwa kwa kanuni za uhuru wa dini, na uhuru kwa wote, na juu ya msingi wa Neno la Mungu la Milele. Bali sisi tumeupotosha huo—siasa. Tumewapigia watu kura chini ya kununua na kuuza na ahadi za uongo, hata taifa letu, na siasa zetu, na demokrasia yetu imechafuka sana hata—imechanganyikana na Ukomunisti na kila namna za "itikadi."

Na mara nyingi tunafanya kwenye baraza la maombi wakati Umoja wa Mataifa unapokutanika mle ndani ama wanapokutana kwa mahojiano. Na katika wakati mmoja mkuu hivi majuzi, hapakuwa na wakati hata mmoja uliotengwa kwa maombi! Tutawezaje kutatua mizozo bila maombi? Tunawezaje kamwe kutarajia ulimwenguni kote kutenda jambo lo lote bila ya uongozi wa Roho Mtakatifu?

Bali hebu niseme jambo hili kwa upendo na heshima kwa taifa letu, na kwa bendera yake, na kwa Jamhuri ambayo inasimamia; tumemkataa Kiongozi wetu, Roho Mtakatifu, na kwa siasa za ufisadi tumewaingiza watu walioharibikiwa na akili. Na msipokuwa macho, watafanya moja ya makosa mabaya sana waliyopata kufanya sasa hivi: ni kwa kuwa wanadamu wanataka mwanadamu atawale.

Tunachohitaji katika ikulu hii ya Marekani kama Rais, tunachohitaji katika Bunge, tunachohitaji katika mahakama yetu ya haki, ni watu ambao wameyaweka wakfu maisha yao kwa Mungu, na wamejazwa na Roho Mtakatifu, nao wanaongozwa na maongozi Yake ya Kiungu. Bali badala ya jambo hilo, tunachagua watu wenye elimu, watu wenye mfano wa utauwa bali wanakana nguvu za Mungu, watu wasioamini kuna Mungu na wakati mwingine wabaya kuliko

hao—tumewaingiza katika mambo ya siasa za taifa letu; si huko tu bali makanisani mwetu.

Makanisa yetu yamepotoka juu ya msingi kwamba sisi, katika kuchagua wachungaji wa kutuongoza, tumeenda kwenye seminari na tumewachagua watu ambao wana elimu kwelikweli, watu ambao ni werevu sana akilini; watu wenye kisomo, nao wanajua kuchanganyikana na watu sana, nao ni watu mashuhuri katika ujirani, jambo ambalo sina neno dhidi yake; watu ambao ni wema katika mienendo yao, waangalifu katika maisha yao, na jinsi wanavyoenenda miongoni mwa binadamu wengine na miongoni mwa watu; watu mashuhuri katika fani zao, jambo ambalo silinenei mabaya—Mungu na anizuie nisiwe mwovu namna hiyo—bali hata hivyo, hicho sicho Mungu alichotuchagulia! Ni uongozi wa Roho Mtakatifu—Kristo ndani ya moyo wa mwanadamu.

Wengi wa hao watu wenye elimu ambao husimama mimbarani na kukana kuwepo halisi kwa Roho Mtakatifu. Wengi wao wanakana kuwepo kwa kuponya Kiungu na nguvu za Roho.

Nilikuwa ninasoma makala jana; (naamini yalikuwa makala) mfululizo wa kato za magazeti kutoka kwa Jack Coe, marehemu Jack Coe, mmoja wa watu niliowavuta kwa Bwana Yesu, aliyekuwa shujaa wa vita katika siku zake, naye alipelekwa mahakamani kule Florida, kwa sababu ya kumwomba mtoto mdogo atoe viatu vyake vya chuma kutoka miguuni mwake na kutembea jukwaani. Na alipofanya hivyo, yule mtoto alitembea jukwaani kama kawaida halafu akaanguka alipomfikia mamaye—zote zikiwa ni jama za yule adui wa Kristo.

Huyu kijana mwanamke na mumewe wakamleta ndugu wetu shujaa kwenye mahakama ya nchi. Na wakati kila kanisa lilipaswa kumtetea Ndugu Jack, wakati kila mtu wa kanisa anayelitaja Jina la Yesu Kristo alipaswa kumuunga mkono kishujaa; kila mtu anayeliita Jina la Bwana Yesu alipaswa kupiga magoti yake katika maombi, bali badala ya jambo hilo, katika vichwa vya magazeti—moja ya madhehebu yetu yaliyo makuu yalisema yameungana na wasioamini kwamba kuna Mungu kumhukumu na kumfunga jela Ndugu Jack Coe. Ungeweza kuwazia kanisa linalojiita kwa Jina la Kristo, lingeungana mikono na wasioamini kwamba kuna Mungu kumhukumu mcha Mungu, ambaye alikuwa anajaribu kwa moyo wake wote kuitetea Biblia? Bali walifanya jambo hilo.

Ndipo Ndugu Gordon Lindsay alienda kumwokoa, na wakati yule hakimu asiyeamini aliposema, “Mtu huyu ni mlaghai, kwa maana alitoa viatu vya chuma kutoka kwa mtoto huyo na kumwacha aende jukwaani, na kusema ameponywa, na

akadanganya na kufanya jambo hilo dhidi ya maagizo ya daktari; kwa hiyo, yeye ana kesi ya ulaghai."

Ndipo Bw. Coe akainuka, akasema, "Bwana, nakanusha tamshi hilo. Mungu alimponya mvulana huyo."

Ndipo hakimu akasema, "Nitamuuliza mtu ye yote katika mahakama haya kama tamshi hilo lingeweza kuwa kweli kwamba Mungu angeweza kuponya kijana huyo kwenye upande mmoja wa jukwaa, na kumwacha awe mgonjwa upande wa pili. Kama tamshi hilo linaweza kuthibitishwa kwa Biblia, basi nasema Bw. Coe ana haki kwa tamshi lake."

Ndipo mhudumu akainua mkono wake akasema, "Mheshimiwa, bwana, naweza kuyasema?"

Naye hakimu akasema, "Endelea."

Basi yule mhudumu akasimama kwa miguu yake akasema, "Usiku mmoja kwenye bahari iliyokuwa inasukasuka, wakati meli ndogo ilikuwa karibu kuzama; matumaini yote ya kuokolewa yalikuwa yamekwisha. Wao walimwona Yesu, Mwana wa Mungu, akija anatembea juu ya maji. Na mmoja wa hao mitume, jina lake Petro, kasema, 'Ikiwa ni Wewe, Bwana, niamuru nije Kwako juu ya maji.' Naye asema . . . Bwana akamwambia huyo mtume, Petro, 'Njoo.' Ndipo akatoka kwenye ile mashua, bwana, akitembea vizuri tu kama Yesu alivyokuwa anatembea juu ya maji. Bali alipoogopa, akaanza kuzama kabla hajafika kwa Yesu."

Yule hakimu akasema, "Kesi imefutiliwa mbali."

Tunahitaji uongozi wa Roho Mtakatifu—si wa watu wenye kisomo.

Sauli, mwana wa Kishi, alifanywa kapteni wa watu wake. Naye akawachukua watu elfu mbili na Yonathani akachukua elfu moja, ndipo Yonathani akashuka akaenda kwenye ngome na kulipiga kundi la Waamori, Waamoni hasa. Na wakati—wakati alipowapiga, Sauli akapiga tarumbeta na kusema, "Mnaona aliyofanya Sauli?" Akaanza kujigamba.

Mara tu mtu anapokuwa Daktari mkuu wa Uungu, ama anapata kitu fulani kidogo nyuma ya jina lake, yeye anakuwa kwa kadiri "mjuvi." Mtu wa Mungu ni mtu mnyenyekevu. Watu wa Mungu ni watu wanyenyekevu.

Unapomwona mtu fulani anayesema wamempokea Roho Mtakatifu na kuanza kujitenga wenyewe, kama kwamba hawana imani, wakienda huku na huko wakijaribu kuwa kitu wasicho, kumbuka tu, wao hawajampokea Bwana Yesu.

Ndipo tunaona ya kwamba adui aliingia, naye alikuwa aingie katika kundi dogo la watu wa Mungu na alikuwa anaenda kuling'oa jicho la mkono wa kulia la kila mtu. Hivyo ndivyo adui daima anavyojaribu kufanya, ni kuyang'oa macho yote mawili kama akiweza, ili kwamba watu wasiweze kuona wanachofanya.

Hivyo ndivyo Shetani anavyojaribu kufanya kwa kila Mkristo—kung'oa macho yake ya kiroho, ili kwamba aweze kufuata tu hisi ya mambo ya kielimu na si hisi ya Roho Mtakatifu anayemwongoza.

Kwa hiyo basi walipofanya jambo hilo, wakati kule kushindwa kukuu kulipokuja, ndipo Sauli alichinja maksai wawili wakubwa na kuwapeleka kwa watu wote. Na laiti mngaliona hapa. Wakati Sauli alipopeleka vipande vya yule maksai kwa Israeli wote na kusema, "Na iwe kwamba mtu ye yote ambaye hatamfuata Samweli na Sauli, na awe (huyu maksai) kama huyu." Mnaona jinsi alivyojaribu kujiwakilisha kwa hila pamoja na mtu wa Mungu? Jinsi lilivyokuwa si la Kikristo. Uchaji wa watu ulikuwa kwa ajili ya Samweli. Bali Sauli akawafanya wote wamfuate kwa maana watu walimcha Samweli. "Na wamfuate Samweli *na* Sauli."

Na ni mara ngapi leo tumesikia eti: "Sisi ni kanisa lililo kuu;" "Sisi ni Church of Christ;" "Sisi ni Church of God;" "Sisi ni *fulani wa fulani*." Inawafanya watu wawe na uchaji na kufikiri ati ni kweli hapo ndipo Mungu anapotenda kazi. Nao hawataki uongozi wa Roho Mtakatifu; afadhali wamfuate mwanadamu kama huyo, kwa maana wao wanapenda kuishi maisha yao wenyewe. Wao hutaka kuamini wanachotaka kuamini.

Mnaona Roho Mtakatifu ndiye Hakimu wetu? Mungu kamwe hakutupa papa, ama askofu, ama mtu ye yote kuwa hakimu. Roho Mtakatifu, ule Utu wa Mungu katika mfano wa Roho Mtakatifu, ni Hakimu wetu na Kiongozi wetu. Sasa mbona hivi?

Tafadhali samahani kwa tamshi hili jeuri na lililo jeuri sana. Simaanishi kuwa bahili; nalisema kwa upendo. Bali Roho Mtakatifu anasema ni kosa kwa wanawake wetu kukata nywele zao, na ni kosa kwa wanawake wetu kuvalia kaptura ndogo na suruali na kujipodoa midomoni na usoni kwa rangi; Roho Mtakatifu anasema ni makosa. Bali tunataka watu watwambie ya kwamba ni sawa!

"Mradi tu tunamfuata mimi na Samweli." Wao wapenda kuishi siku sita jinsi watakavyo, wanaenda kanisani Jumapili asubuhi—nao ni wanachuoni bora, waliohitimu chuoni na digrii nyingi, wanaweza kuwazungumzia somo dogo ambalo . . . utani mchache ambao utayafurahisha maskio yao na kuwatumbuiza kama vipindi fulani vya sinema ama televisheni, na kukariri ombi dogo juu yao, na kuwatuma nyumbani wakiwa na usalama wa kujiridhisha wenyewe ya kwamba wametekeleza dini yao.

Hayo si mapenzi ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anakutaka uishi kitauwa kila siku katika juma na kila usiku, ukijitenga na mambo ya ulimwengu. Bali kanisa halitaki jambo hilo. Wao wanataka mtu anayeweza kuifasiri Biblia jinsi wanavyotaka kusikia. Wao hawataisikiliza Sauti ya Roho Mtakatifu ikinena kupitia kwenye Biblia.

Wengi wao wanataka kusema, “Siku za miujiza zimepita.” Hilo ndilo linalowafurahisha watu. Wao wanataka kusema, “Hakuna ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Watu hawataki kutenda tofauti na jinsi walimwengu wengine wanavyofanya. Hawataki kwenda mitaani na kunawa nyuso zao, na watu wenye nyuso safi na bila sigara midomoni mwao, na misokoto, na viko, na mambo wanayofanya wanaume; nao wanawake wanataka kukata nywele zao ziwe fupi sana na kuvalia nguo ndogo, zinazoonyesha umbo lao na mambo wanayotaka. Wao—wao wanataka mtu atakayewaambia ya kwamba hayo ni sawa.

Ndipo hivi majuzi usiku akaja mtu kuniambia ya kwamba ati kwa sababu nilikuwa nimehubiri dhidi ya mambo hayo, ya kwamba madhehebu fulani makubwa, kama matano hivi, yalisema, “Tutaachana na Ndugu Branham na tusiwe na uhusiano wo wote naye tena. Aidha utaagiza kanda hizo zirudishwe na kuomba msamaha kwa ajili yazo, ama tutaachana nawe.”

Nikasema, “Nitasimama na Neno la Mungu hata ikinigharimu kila kitu kilicho ndani ya maisha yangu. Nitabaki na Neno nami . . . ”

Kasema, “Vema, si ni afadhali uagize kanda *fulani na fulani* zirudishwe?”

Nikasema, “Sijahubiri cho chote maishani mwangu ambacho nilionea aibu. Mimi sitaagiza kanda zo zote zirudishwe, wala rekodi zo zote. Nitadumu na anayosema Roho Mtakatifu. Hayo nitaishi nayo na kufa nayo.” Mimi sijaribu kuzungumzia juu yangu binafsi, sasa, bali ninajaribu tu kuwapa mfano wa yanayoendelea kusudi mpate kuona na kufahamu. Ni watu kutaka kuongozwa na mwanadamu.

Wao hawakumtaka Samweli. Ndipo kabla hawajamtia mafuta Samweli kuwa mfalme, ama Sauli kuwa mfalme, samahami, Samweli akawajia tena. Nami nitazungumza katika lugha ambayo angelitumia leo. Mnaweza kuyasoma.

Yeye alisema, “Kuna ubaya gani kwa Mungu kuwa Mfalme wenu?”

“Vema, hatumwoni Mungu.”

“Vema, mimi ni mwakilishi Wake.” Samweli akasema, “Mimi nimewahi kuwaambia jambo lo lote ambalo ni makosa? Nimewahi kutabiri cho chote ambacho hakikutimia kama nilivyosema kingetimia? Si mimi nimewaambia Neno la Bwana? Nami nitawaulizeni jambo hili: Nimeshawajia ninyi na kuomba fedha zenu zo zote? Nimewahi kuchukua cho chote kutoka kwenu? Nimewahi kuwaletea cho chote ila moja kwa moja BWANA ASEMA HIVI? Na Mungu amelithibitisha kila mara kuwa ilikuwa Kweli, na ametuma mvua ya ngurumo na mvua.” Mnajua Maandiko na mko pale pale kuthibitisha ya kwamba Samweli alikuwa msemaji wa Mungu.

Na kama vile Samweli alivyomwakilisha Roho Mtakatifu leo kikamilifu leo. Roho Mtakatifu ni Msemaji wa Mungu. Ambaye hunena yale hasa iliyosema Biblia. Ambaye anaamini yale hasa Biblia ilisema na hatayaghairi hata kidogo, bali wao walitaka mtu ambaye angewaambia vinginevyo.

Na hao watu hawangalisema ya kwamba unabii wa Samweli haukuwa mkamilifu. Wao walijibu na kusema, "Samweli, yote uliyonena katika Jina la Bwana, Bwana ameyatimiza kama tu vile ulivyosema. Hakuna hata kosa moja ndani yake. Wewe hujawahi kuja kwetu na kutuomba fedha zetu. Wewe umejilisha mwenyewe. Hujawahi kutuomba kukufanyia jambo lo lote kubwa. Wewe umemtumaini Mungu wako, naye amekuokoa na mambo yote. Na maneno yako ni kweli—kila kitu ulichonena katika Jina la Bwana kimetimia kama tu ulivyosema, bali hata hivyo tunataka mfalme!"

Mnaweza kuona hitilafu? Mna—mnaweza kuona ule—ule ujanja wa ibilisi unavyoweza kutenda kazi katika mwanadamu? Badala ya mwanamume kujitoa mwenyewe, ama mwanamke, kwa Roho Mtakatifu na kusikiza BWANA ASEMA HIVI ni nini kwa ajili ya maisha masafi, utu usioghoshiwa, kwa ajili ya maisha tofauti, watu wa kipekee, taifa takatifu, watu wanaotenda kipekee, wao waliona afadhali wafanane na walimwengu, watende kama walimwengu, na kuhudhuria makanisa fulani yanayosema, "Hiyo ni sawa; ninyi fanyeni tu hayo na mwendelee."

Mnaweza vile ilivyo? Wao wanasema, "Hakuna kitu kama kuponya. Loo, ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa mjengo wa kanisa." Kwa maneno mengine, basi Mungu alimchukua mtu, akamtoa Roho Mtakatifu kanisani na kuyaachia madhehebu yalijenge. La, hasha. Hakuna kitu kama hicho. Roho Mtakatifu, Neno la Kweli, alikuwa awaongoze hata atakapokuja Yesu. Bali hivyo ndivyo i—ilivyotukia.

Sauli akaja mamlakani. Alikuwa na wafuasi wengi. Loo, alikuwa na silaha nzuri; alikuwa na waimbaji; alikuwa na ngao; na alikuwa na mikuki. Loo, yeye alikuwa bora kuliko mataifa mengine yote. Naye akawaingiza kwenye demokrasia ambayo ilikuwa zaidi ya kitu cho chote ambacho mtu ye yote alipata kusikia.

Na hayo ndiyo hasa madhehebu yetu na makanisa yamefanya leo. Tuna majengo makubwa sana ya kanisa ulimwenguni. Tuna watu waliovalia vizuri sana ulimwenguni. Tuna elimu ya hali ya juu sana inayoweza kuletwa. Kama wale watu wa Sauli waliofunzwa ambao wangechukua mkuki huo, nao wangaliutupa na kuutumia hata mataifa yakawaogopa. Walikuwa watu waliofunzwa, na kadhalika.

Bali siku moja, kukatokea wakati ambapo kulitokea usai. Nao ulilihangaisha jeshi lote la Israeli hata likasimama

likitetemeka katika viatu vyao. Goliathi aliwasai: “Kama Mungu wenu yuko vile mnavyosema alivyo, ninyi mmefunzwa vizuri sana,” naye akawasai. Wao hawakujua la kufanya. Silaha zao zilizopigwa msasa hazingefaa. Mikuki yao haingefaa. Kuna jambo lililokuwa linatendeka ambalo wao hakuwa wamelisikia hapo awali. Na kwa uchaji wote, na heshima ya kiungu, na heshima, na uungwana na upendo, na ushirika wa Kikristo, nasema jambo hili; nilisoma hivi majuzi katika gazeti la Kiafrika mahali ambapo mwana wetu wa Kishi, msai wetu wa kiinjilisti—wakati Mwislamu alimsai—Billy Graham—kasema, “Kama mungu wenu ni Mungu, hebu na awaponye wagonjwa kama alivyosema atafanya!” Naye huyo mwana wa Kishi, na jeshi hilo lingine, wakajinyamazia na kuondoka nchini huku wameshindwa. Ni fedheha. Mungu wetu ni Mungu!

Tuna makanisa yetu mazuri; tuna uinjilisti wetu ulio bora; tuna waimbaji wetu wanaolipwa mshahara; tuna kwaya ziliyo bora sana, minara iliyochongoka juu sana nchini; tuna watu walio bora sana, fedha nyingi mno. Tuna wenye elimu; tuna theolojia kern kern; tunaweza kuihubiri; tunaweza kuitangaza; tunaweza kufanya uinjilisti na kuwaleta watu na kuwavuta mamilioni kila mwaka na kuwaingiza kanisani. Waimbaji wetu wanaolipwa mshahara, uinjilisti wetu wa kielimu haujui jinsi ya kukabiliana na usai kama huo. Hawajui kitu juu yake. Hawajui kitu juu ya nguvu Zake za kuponya, za ubatizo wa Roho Mtakatifu, wa nguvu ambazo zinaweza kukichukua kivuli cha mtu anayekufa kwa kansa na kumweka huru. Hawhawajkitu juu yake. Wao hawajafunzwa katika fani hiyo, kama vile Sauli na kundi lake lililoundwa na wanadamu lilivyokuwa.

Bali hebu niwaambie watu wa Mungu na ninyi watoto, kusudi mjue ya kwamba Mungu kamwe hawaachi bila shahidi; bila ya Sauli kujua; Sauli hakujua kitu juu yake, Mungu alikuwa na maskini Daudi kule nyuma ya kilima mahali fulani ambaye hakuwa akiwalisha kondoo magugu ya kidini. Yeye alikuwa anawaongoza kando ya maji ya utulivu na malisho ya majani mabichi! Alikuwa anawajali kondoo wa baba yake, na kama kitu kiliingia (adui) kumnyakua mmoja wa kondoo wa baba yake, yeye alijua nguvu za Mungu za kumwokoa yule kondoo!

Mungu angali ana Daudi mahali fulani ambaye anajua maana ya kumkomboa kondoo wa Mungu kwa nguvu za Mungu. Yeye angali anajua yote juu yake. Yeye alitumaini . . . Yeye hakujua kitu juu ya silaha za Sauli wala hakutaka yo yote yake. Yeye hakutaka yo yote ya madhehebu yao; hakutaka silaha hizo za kale juu yake. Alisema, “Mimi sijui kitu juu yake! Bali hebu mimi niende katika Nguvu ninayoifahamu.”

Yeye alikuwa amewalisha kondoo wa baba yake. Alikuwa ameyalinda malisho. Alikuwa amewapa chakula kinachofaa, nao waliishi na kufanikiwa. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu ndivyo

atakavyoishi mtu." Mchungaji wa kweli huwalisha—"Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele." Na kama adui akimnyakua mmoja katika magonjwa, yeye anajua nguvu za Mungu.

Mwangalie maskini Daudi, alisimama pale. Kasema, "Jamaa yule ni shujaa wa vita tangu alipozaliwa. Na tangu utoto wake hajui kitu ila mkuki na silaha. Yeye amefunzwa vizuri. Yeye ni mwanatheolojia. Nawe hujui kitu juu yake."

Akasema, "Hiyo ni kweli, bwana. Mimi sijui kitu kuhusu mafunzo yake ya kitheolojia, bali kuna jambo moja nijualo: ya kwamba adui alipokuja kumchukua mmoja wa kondoo wa baba yangu, nilienda kwa nguvu za Mungu. Nikamwokoa! Nilimrudisha salama katika afya njema tena. Nilimrudisha tena kwenye kivuli cha malisho yenye majani mabichi na maji ya utulivu. Na Mungu ambaye alimtia yule simba mikononi mwangu, na nikamuua alipochukua mmoja wa wanakondoo wangu, kisha akaniwezesha kumwua yule dubu; kwa hiyo Mungu wa mbinguni ataambatana nami kumwua huyu Mfilisti asiyetahiriwa!" Tunahitaji uongozi wa Roho Mtakatifu.

Sijui siku zangu. Hakuna ajuaye.

Hivi majuzi asubuhi nilikuwa nimelala kitandani mwangu. Nami nilikuwa . . . nilikuwa nimelala, nami nikaota ya kwamba Joseph ni mgonjwa, nami nilikuwa nimemchukua kusudi nimwombee. Na nilipoamka nilikuwa nimefadhaika sana. Nikasema, "Vema, labda Joseph atakuwa mgonjwa." Nami nikatazama na mbele yangu kulikuweko na kivuli kidogo cheusi kikienda, kwa namna fulani chenye rangi ya hudhurungi, na ilionekana kama kwamba kilikuwa ni mimi. Nami nikakitazama na kilikuwa kimefuatwa na mtu mweupe, na ilikuwa ni Yeye. Nikamtazama mke wangu kuona kama alikuwa ameamka kusudi nimwonyeshe; kama angaliweza kuona lile ono, bali alikuwa amelala. Nikasema, "Loo, ninasikitika, Bwana, lakini hayo yamekuwa maisha yangu. Imekulazimu kunisukuma kwenye kila kitu nilichofanya. Kila wakati kitu cho chote kingetukia, ningefikiri ilikuwa ni Wewe unakifanya, nami natambua ilikuwa Shetani akijaribu kunifanya nisikikaribie." Nikasema, "Laiti Wewe ungeliniongoza tu." Na nilipoangalia niliona uso mzuri sana niliopata kuona katika mtu. Alikuwa mbele yangu akiangalia nyuma. Akainua mkono Wake na kuushika wangu akaanza kwenda hivi. Hilo ono likaniacha.

Jumapili iliyopita niliamka mapema. Hiyo ilikuwa Jumamosi; ono hili. Daima nimefadhaika. Daima nimefikiri juu ya kufa. Mimi, nikiwa na umri wa miaka hamsini, wakati wangu si . . . Sidhani ilikuwa muda mrefu sana. Sijui nitakavyokuwa katika mwili huu wa Kiungu—mwili wa kimbinguni. Je! ingekuwa kwamba ningewaona marafiki wangu wapendwa na kuona ukungu mdogo ukipita na kusema, "Huyo hapo Ndugu

Neville anaenda," ama hangaliweza kusema, "Aloo, Ndugu Branham"? Na wakati Yesu alipokuja, ndipo ningekuwa mtu tena. Nilifikiria jambo hilo mara kwa mara.

Nilikuwa ninaota ya kwamba nilikuwa huko magharibi nami. . .nilikuwa ninashuka nikija kupitia kwenye kijiti cha majani, na mke wangu alikuwa pamoja nami, nasi tulikuwa tumetoka kuvua samaki mtoni. Nami nikasimama nikafungua lango, na anga zilikuwa nzuri sana. Haikuonekana kama vile ilivyo hapa bondeni. Yalikuwa mawingu mazuri ya samawati na meupe. Ndipo nikamwambia mke wangu, nikasema, "Ilitubidi kuwa huku nje mapema sana, Mpenzi."

Yeye akasema, "Kwa ajili ya watoto, ilitupasa tuweko, Billy."

Nikasema, "Hiyo . . . " Nami nikaamka. Nikawaza, "Ninaota sana. Sijui kwa nini." Nami nikaangalia chini naye alikuwa amelala karibu nami. Basi nikainuka kwenye mto wangu, kama vile wengi wenu enyi watu mmefanya. Nikaweka kichwa changu kwenye ubao wa kichwani wa kitanda na kuweka mikono yangu nyuma yangu. Nami nilikuwa nimelala pale namna hii kisha nikasema, "Vema, sijui tu jinsi itakavyokuwa, nga'mbo ya pili. Mimi tayari nina umri wa miaka hamsini, nami sijafanya kitu bado. Laiti ningalifanya kitu fulani tu kumsaidia Bwana. Kwa maana najua sitakuwa anayepatikana na mauti. . .Nusu ya wakati wangu imepita, lakini, ama zaidi ya nusu. Kama nikiishi kuwa na umri wa watu wangu, hata hivyo nusu ya wakati wangu imekwisha. Nami nikaangalia kila mahali na nilikuwa nimelala pale nikijaribu kuamka. Ilikuwa kama saa 1:00. Nikasema, "Naamini nitashuka niende kanisani asubuni ya leo. Kama nikipwelewa na sauti, ningetaka kumsikia Ndugu Neville akihubiri."

Kwa hiyo, nikasema, "U macho, Mpenzi?" Naye alikuwa amelala fofofo.

Basi sitaki mlikose jambo hili. Limenibadilisha. Siwezi kuwa Ndugu Branham yeye yule niliyekuwa.

Ndipo nikaangalia, nami nikasikia kitu kilichoendelea kusema, "Umeanza tu. Piga vita. Endelea kukaza mwendo."

Nikakitikisa kichwa changu kidogo kisha nikawaza, "Vema, labda ninawazia tu namna hii, mwajua, mtu anaweza kupata mawazo," nami nikasema, "labda niliwazia hayo tu hayo."

Ikasema, "Piga vita! Endelea kusonga mbele! Endelea kusonga mbele!"

Nami nikasema, "Labda mimi nilisema jambo hilo."

Nami nikaweka midomo yangu kwenye meno yangu, na kuweka mkono wangu juu ya kinywa changu, na hiyo hapo ikaja tena. Kasema, "Endelea tu kukaza mwendo. Laiti ungalijua kilichokuwa kwenye mwisho wa safari." Na ilionekana kana kwamba ningemsikia Graham Snelling ama mtu fulani ambaye

aliimba ule wimbo namna hii; wao wanaouimba hapa—Anna Mae na wengine wenu nyote:

> Nina hamu ya kwetu sana na nina huzuni na nataka kumwona Yesu;
> Ningetaka kusikia hizo kengele za bandari zikilia;
> Ingeangaza njia yangu na kutowesha hofu zote;
> Bwana, hebu niangalie ng'ambo ya pazia la wakati.

Mmeusikia ukiimbwa hapa kanisani.

Nami nikasikia kitu kikisema, "Ungetaka kuangalia ng'ambo ya pazia?"

Nikasema, "Lingenisaidia sana." Nami nikatazama, na katika dakika moja, ni. . .kupumua mara moja, nilikuwa nimefika mahali padogo ambapo paliinama. Nikatazama nyuma, nami huyo pale nimelala kitandani. Ndipo nikasema, "Hili ni jambo la ajabu."

Sasa, nisingewataka ninyi mrudie jambo hili. Hili ni mbele ya kanisa langu, ama kondoo wangu ninaowachunga. Ama ilikuwa kwamba nilikuwa katika mwili ama nje yake, ama ilikuwa kuhamishwa. . .Haikuwa kama ono lo lote nililopata kuona. Ningeangalia pale, na ningeliangalia hapa. Na nilipofika mahali pale padogo, sijawahi kuona watu wengi hivi wanaokuja mbio, wakipiga kelele, "Loo, ndugu yetu wa thamani." Nami nikaangalia, na vijana wanawake, labda kwenye umri usiozidi sana miaka ishirini (kumi na minane hadi ishirini) walikuwa wananikumbatia na kupiga kelele, "Ndugu yetu wa thamani."

Huyu hapa kijana anakuja katika uangavu wa utu uzima, na macho yao yanang'ara na kuonekana kama nyota katika usiku wenye giza, meno yao meupe kama lulu, nao walikuwa wakipiga kelele na kunishika ghafla na kupiga kelele, "Loo, ndugu yetu wa thamani." Nami nikasimama na kutazama, nami nilikuwa kijana. Nikaangalia nyuma kwenye mwili wangu mzee umelala pale na mikono yangu nyuma ya kichwa changu. Basi nikasema, "Sielewi jambo hili." Na hawa vijana wanawake wakinikumbatia kwa mikono yao.

Naam, natambua ya kwamba huu ni umati uliochanganyikana, nami nasema hili kwa utamu na uzuri wa Roho. Wanaume hawawezi kuwakumbatia wanawake bila ya msisimko wa kibinadamu. Lakini haukuwepo. Hapakuwepo na jana wala kesho. Wao hawakuchoka. Wao walikuwa. . . Sijapata kuona wanawake warembo jinsi hiyo maishani mwangu mwote. Nywele zao zilikuwa zimefika hata kiunoni, rinda ndefu zilizofika miguuni, nao walikuwa wakinikumbatia tu. Hakikuwa kikumbatio kama kile ambacho hata dada yangu anayeketi pale angenikumbatia. Hawakuwa wakinibusu, nami sikuwa nikiwabusu. Kilikuwa kitu ambacho sina msamiati;

sina maneno ya kusema. *Ukamilifu* halingeligusa. Kipeo hata halingaliligusa po pote. Kilikuwa kitu ambacho kamwe sija-. . . Itakubidi tu kuwa kule.

Nami nikatazama huku na huko, nao walikuwa wakija kwa maelfu. Nami nikasema, “Sifahamu jambo hili.” Nikasema, “Mbona wao . . .” Na huyu hapa Hope anakuja—huyo alikuwa mke wangu wa kwanza. Yeye alikimbia na hakusema kamwe, “Mume wangu.” Alisema, “Ndugu yangu mpendwa.” Na wakati aliponikumbatia, palikuwepo na mwanamke mwingine amesimama hapo aliyekuwa amekwisha nikumbatia, ndipo Hope akamkumbatia mwanamke huyu, na kila mmoja . . .

Nami nikafikiri, “Loo, hili halina budi kuwa ni jambo tofauti, haiwezekani. Kuna kitu . . . Loo, ningalitaka kamwe kurudi kwenye maskini mzoga ule tena?” Nikaangalia kila mahali pale na kuwaza, “Ni nini hii?” Nami nikaangalia kwa makini sana, ni—nikasema, “Si—siwezi kufahamu jambo hili.” Bali Hope alionekana kama . . . loo mgeni wa heshima. Hakuwa tofauti lakini kama tu mgeni wa heshima.

Ndipo nikasikia sauti wakati huo iliyonena nami iliyokuwa chumbani, kasema, “Hii ndiyo uliyohubiri kuwa ni Roho Mtakatifu. Huu ndio upendo makamilifu. Na hakuna kinachoweza kuingia humu bila huo.”

Nimeazimia sana kuliko wakati wo wote maishani mwangu ya kwamba inahitaji upendo mkamilifu kuingia mle. Hapakuwa na wivu. Hakukuweko na uchovu. Hakukuweko na mauti. Magonjwa hayangeweza kuingia mle. Kupatikana na mauti hakungeweza kukufanya mzee, nao hawangeweza kulia. Ilikuwa tu furaha moja—“Loo, ndugu yangu mpendwa.”

Nao wakanichukua na kuniweka juu ya mahali pamoja pa juu. Nami nikawaza, “Mimi sioti ndoto. Ninaangalia kule nyuma kwenye mwili wangu uliolala kule chini kitandani.” Nao wakaniweka mimi pale nami nikasema, “Loo, hainipasi kuketi hapa juu.”

Na hapa wakaja wanawake na wanaume kutoka pande zote mbili katika tu ukamilifu wa ujana, wanapiga kelele. Na mwanamke mmoja alikuwa amesimama pale naye akapiga kelele, “Loo, ndugu yangu mpendwa. Loo, tunafurahi kukuona hapa.”

Nikasema, “Mimi sifahamu jambo hili.”

Ndipo sauti hiyo iliyokuwa ikinena nami kutoka juu yangu, ikasema, “Unajua imeandikwa katika Biblia ya kwamba manabii walikusanywa pamoja na watu wao.”

Nami nikasema, “Naam, nakumbuka jambo hilo katika Maandiko.”

Kasema, “Lakini, huu ni wakati utakapokusanyika pamoja na watu wako.”

Nikasema, "Basi watakuwa halisi, nami naweza kuwahisi." "Naam, ndiyo."

Nikasema, "Lakini mimi . . . Kuna mamilioni. Hakuna Wabranham wengi namna hiyo."

Na sauti hiyo ikasema, "Hao si Wabranham; hao ni wale uliowavuta. Hao ndio ambao uliowaongoza kwa Bwana." Kisha kasema, "Baadhi ya hao wanawake pale unaofikiri ni warembo sana walikuwa na zaidi ya miaka tisini ulipowaongoza kwa Bwana. Si ajabu wao wanapiga kelele, 'Ndugu yetu mpendwa.'"

Nao wakapiga kelele mara moja, kasema, "Kama haungalikwenda, hatungalikuwa hapa."

Nikaangalia kila mahali nikawaza, "Vema, sifahamu." Nikasema, "Loo, Yuko wapi Yesu? Nataka kumwona vibaya sana."

Wao wakasema, "Naam, Yuko juu kidogo tu, moja kwa moja upande ule." Kasema, "Siku moja Yeye atakuja kwako." Mnaona? Kasema, "Wewe ulitumwa kuwa kiongozi na Mungu atakuja, na atakapokuja, Yeye atakuhukumu kulingana na yale uliyowafundisha, kwanza; kama wataingia ama hawataingia. Tutaingia kulingana na mafundisho yako."

Nikasema, "Loo, ninafuraha sana! Je, Paulo—yeye itambidi kusimama namna hii? Itambidi Petro kusimama namna hii?"

"Naam."

Nikasema, "Basi nilihubiri kila neno walilohubiri. Sikuhitilafiana kutoka upande mmoja kwenda mwingine. Walipobatiza katika Jina la Yesu Kristo, nilibatiza pia. Walipofundisha ubatizo wa Roho Mtakatifu, nilifundisha pia. Kila walichofundisha, nilifundisha pia."

Ndipo hao watu wakapiga kelele wakasema, "Tunajua jambo hilo, nasi tunajua tunarudi pamoja nawe siku moja duniani." Kasema, "Yesu atakuja, nawe utahukumiwa kulingana na Neno ulilotuhubiria sisi. Halafu, kama ukikubalika wakati huo, ambapo utakubalika," kisha kasema, "basi wewe utatukabidhi Kwake kama tunu yako ya huduma yako." Kasema, "Utatuongoza Kwake na sote pamoja tutarudi duniani tukaishi milele."

Nikasema, "Inanibidi kurudi kule sasa?"

"Ndiyo, bali endelea kukaza mwendo."

Nikaangalia, nami ningeweza kuwaona hao watu; umbali nilioweza kuona, wangali wanakuja, wakitaka kunikumbatia, wakipiga kelele, "Ndugu yetu mpendwa."

Mara sauti ikasema, "Kila ulichowahi kupenda, na kila kilichowahi kukupenda, Mungu amekupa wewe hapa." Nami nikaangalia na huyu hapa mbwa wangu wa zamani anakuja. Huyu hapa farasi wangu anakuja na kukilaza kichwa chake

juu ya bega langu na kulia. Kasema, “Kila ulichowahi kupenda na kila kilichowahi kukupenda, Mungu amevikabidhi mikononi mwako kupitia kwa huduma yako.”

Nami nikajisikia nikitoka mahali hapa pazuri. Ndipo nikaangali kila mahali. Nikasema, “U macho, Mpenzi?” Alikuwa angali analala. Nami nikawaza, “Ee Mungu, loo nisaidie, ee Mungu. Usiniache kamwe nipatane kwa neno moja. Nijalie nidumu sawasawa katika Neno hilo na kulihubiri. Sijali nini kinachokuja ama kinachokwenda, kile mtu ye yote afanyacho, ni Sauli wangapi ama wana wa Kishi watainuka, ni wangapi *hawa, wale,* na *wengineo*, nijalie mimi, Bwana, kukaza mwendo nipafikie mahali pale.”

Hofu yote ya mauti . . . Nasema jambo hili huku Biblia yangu ikiwa mbele zangu asubuhi ya leo. Nina kijana mdogo pale, mwenye umri wa miaka minne, wa kulea. Nina msichana mwenye umri wa miaka tisa na msichana tineja ambao ninashukuru kwa ajili yao, ambao wameishika njia ya Bwana. Mungu na anijalie niishi nipate kuwalea katika maonyo ya Mungu. Juu ya hayo, inaonekana kama kwamba ulimwengu mzima unanipigia kelele. Wanawake na wanaume wenye umri wa miaka tisini na wa namna zote, “Kama usingelienda, hatungalikuwa hapa.” Basi Mungu anijalie kupiga vita. Lakini kama ikifikia kufa, mimi si ninino zaidi . . . Ingekuwa ni furaha, ingekuwa furaha kuingia kutoka upotovu huu na aibu.

Kama ningalifanya kule ng’ambo, maili bilioni mia moja kwenda juu, kipande cha mraba, na hicho ni upendo mkamilifu. Kila hatua upande huu, inasonga, hata tunapofikia mahali tulipo sasa. Ingekuwa tu ni kivuli cha upotovu. Hicho kitu fulani kidogo tunachoweza kuhisi na kusikia ya kwamba kuna kitu fulani mahali fulani; hatujui ni nini. Loo, rafiki zangu wapendwa, wapendwa wangu, wapenzi wangu wa Injili, watoto wangu niliomzalia Mungu, nisikizeni mimi, mchungaji wenu. Ninyi . . . Laiti kungalikuwa na njia ningaliweza kuwaelezea ninyi. Hakuna maneno. Nisingeyapata. Hayako po pote. Bali ng’ambo tu ya huku kupumua kwa mwisho ni jambo lenye utukufu sana nililowahi . . . Hamna njia ya kulielezea. Hamna njia; siwezi tu kufanya hivyo. Bali cho chote ufanyacho, rafiki, weka kando kila kitu hata utakapopata upendo mkamilifu. Fikia mahali ambapo unaweza kumpenda kila mtu, kila adui, cho chote kile. Huko kuzuru kwangu kumoja kule kumenifanya mtu tofauti. Siwezi kamwe, kamwe, kamwe kuwa Ndugu Branham yeye yule niliyekuwa.

Hata kama ndege zinatikisika, ambapo umeme unamemetesha, hata kama majasusi wamenilenga bunduki, hata iwe nini, haidhuru. Mimi nitapiga vita kwa neema ya Mungu huku nimehubiri Injili kwa kila kiumbe na kila mtu niwezaye, nikiwashawishi waingie katika ile nchi nzuri kule

ng'ambo. Inaweza kuonekana ngumu; inaweza kuhitaji nguvu nyingi.

Sijui itachukua muda gani tena. Hatujui. Kuzungumza kimwili, kutokana na kuchunguzwa kwangu hivi majuzi, kasema, "Una miaka 25 ya maisha mazuri na ya kazi ngumu. Wewe ni mzima kabisa." Jambo hilo lilinisaidia. Bali loo, halikuwa hilo. Hilo silo. Ni kitu fulani ndani *humu*. Huu uharibikao hauna budi kuvaa usioharibika; huu unaopatikana na mauti hauna budi kuvaa usiopatikana na mauti.

Wana wa Kishi wanaweza kuinuka. Nina . . . mambo yote mazuri wafanyayo, sina jambo baya la kusema juu yake; kuwapa maskini na kufanya fadhili. Basi kumbukeni, mbona, Samweli alimwambia Sauli, "Utatabiri pia." Na wengi wa watu hao ni wahubiri wakuu mno na wenye nguvu, wanaweza kulihubiri Neno kama malaika wakuu, bali hata hivyo haikuwa mapenzi ya Mungu. Mungu alipaswa awe Mfalme wao. Basi ndugu, dada, acha Roho Mtakatifu akuongoze. Hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu.

> Nina hamu ya kwetu sana na nina huzuni na nataka kumwona Yesu;
> Ningetaka kusikia hizo kengele tamu za bandari zikilia;
> Ingeangaza njia yangu na kutowesha hofu zote;
> Bwana, hebu tuangalie ng'ambo ya pazia la wakati.
>
> Bwana, hebu niangalie ng'ambo ya pazia la huzuni na hofu;
> Hebu niiangalie hiyo nchi yenye jua na inayong'aa.
> Ingetia nguvu imani yetu na kutowesha hofu zote;
> Bwana, hebu na waangalie ng'ambo ya pazia la wakati.

Nina hakika, Bwana, kama kanisa hili dogo, asubuhi ya leo, lingaliangalia tu ng'ambo ya pazia. Hakuna mateso miongoni mwao, wala hayangeweza kuwepo. Hamna maradhi, hamna kitu ila ukamilifu— na ni kupumua mara moja tu kati ya hapa na kule—kutoka uzeeni kuingia ujana, kutoka katika wakati kuingia Umilele. Kutoka uchovu wa kesho na huzuni ya jana hata wakati uliopo wa Umilele, katika ukamilifu.

Ninaomba, Mungu, ya kwamba utambariki kila mtu hapa. Kama kuna wale hapa, Bwana, ambao hawakujui katika njia ya upendo . . . Na kweli, Baba, hakuna kingaliweza kuingia Mahali hapo Patakatifu bila upendo wa namna hiyo; kule kuzaliwa upya kuzaliwa mara ya pili. Roho Mtakatifu—Mungu, ni upendo. Nasi tunajua ya kwamba jambo hilo ni kweli. Haidhuru hata kama tukiihamisha milima kwa imani yetu, kama tulifanya mambo

makuu, hata hivyo pasipo huo mle, hatungaliweza kupanda ile ngazi kuu kule ng'ambo. Bali tukiwa na huo, utatuinua juu zaidi ya masumbuko ya dunia hii.

Naomba, Baba, ya kwamba utawabariki hawa watu hapa, na jalia kwamba kila mtu ambaye amenisikia mimi asubuhi ya leo nikisimulia Ukweli huu, ya kwamba upate kuwa shahidi wangu, Bwana. Kama Samweli wa kale, "Nimewahi kuwaambia cho chote katika Jina Lako ila kilichokuwa kweli?" Wao ndio mahakimu. Nami nawaambia leo, Bwana, ya kwamba Wewe umenipeleka kwenye ile Nchi. Nawe wajua ya kwamba ni kweli. Na sasa, Baba, kama kuna wengine wasiokujua Wewe, jalia hii iwe saa watakayosema, "Bwana, weka ndani yangu hiari ya kuwa mapenzi Yako." Tujalie, Baba.

Na sasa huku mmeviinamisha vichwa vyenu, mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, "Niombee, Ndugu Branham. Mapenzi ya Mungu ndani yangu."

Sasa, wakati ukiwa papo hapo ulipo, kwa utamu kabisa, mbona usimwambie Baba, "Mungu, ndani ya moyo wangu, leo nayakataa mambo yote ya ulimwengu. Ninayakataa mambo yote nipate kukupenda na kukutumikia Wewe maishani mwangu mwote. Nami, tangu leo hii na kuendelea, nitakufuata Wewe katika kila Andiko la Biblia Yako." Kama hujabatizwa katika ubatizo wa Kikristo, "Nitabatizwa, Bwana. Kama sijampokea Roho Mtakatifu bado. . . " utajua utakapompokea Yeye. Atakupa, atakupa matumaini na upendo unaohitaji. Loo, huenda ulifanya vinginevyo—ukawa na hisi, kama vile ungalipiga kelele ama ukanena kwa lugha, ambalo ni sawa, bali kama huo Upendo wa Kiungu haumo mle . . . niaminini, sasa.

Sema, "Bwana, weka ndani ya moyo wangu na nafsini mwangu kufikiwa na Roho Wako ili kwamba nipate kukupenda na kukuheshimu na nipate huo Upendo wa Kiungu moyoni mwangu leo ambao ungenipeleka kwenye ile nchi wakati pumzi yangu ya mwisho itakaponitoka." Tunapoomba, waweza kuomba wewe mwenyewe, sasa. Katika njia yako mwenyewe, omba. Mwombe Mungu afanye jambo hilo kwa ajili yako. Nawapenda. Nawapenda. Wewe mtu wa thamani mwenye nywele zenye mvi unayeketi hapa, ambaye umejitahidi na kuwalisha watoto wadogo. Ninyi maskini akina mama wazee ambao mliyafuta machozi machoni mwao. Hebu nikuhakikishie jambo hili, dada mpendwa, si hivyo ilivyo kule ng'ambo ya kupumua kwingine. Naamini kumo kabisa humu chumbani. Ni kiwango tu tunachoishi ndani yake; huu ni upotovu tu ambao tunaishi ndani yake sasa. "Lakini mapenzi Yako ndani yangu, Bwana, mapenzi Yako yatendeke." Wewe omba tunapoomba pamoja.

Kwa kicho, Bwana, juu ya msingi wa Neno Lako na Roho Wako Mtakatifu, tunashukuru sana ya kwamba tunajua mahali

kuzaliwa kwetu kunakotoka. Tunashukuru kwamba tulizaliwa, si kwa mapenzi ya mwanadamu, wala mapenzi ya mwili, bali mapenzi ya Mungu. Nasi tunaomba leo, Baba, ya kwamba hawa ambao sasa wanaomba neema ya msamaha, ya kwamba Roho Wako atafanya kazi hiyo, Bwana. Hakuna njia kwangu kufanya jambo hilo. Mimi ni mwanadamu tu; mwana mwingine wa Kishi. Bali tunakuhitaji Wewe, Roho Mtakatifu. Mungu, jalia niwe kama Samweli—mtu ambaye husema kweli ya Neno. Nawe umelithibitisha umbali huu, nami naamini ya kwamba utaendelea mradi tu nitadumu mwaminifu Kwako.

Wote na waupokee Uzima wa Milele sasa, Baba. Siku hii na isiondoke kwao. Na saa ambayo wao watakuja kuuacha ulimwengu huu, naomba kwamba haya, yale ambayo ndiyo kwanza niwaambie, yawe halisi. Na tunapoketi hapa watu wanaopatikana na mauti, leo, tukiangalia saa zetu, tukifikiria juu ya chakula chetu cha jioni, juu ya kazi kesho, juu ya masumbuko na kazi za maisha, hayatakuwa wakati huo. Yote hutoweka. Hakutakuwa na masumbufu—furaha moja kuu ya Umilele. Wape Maisha ya namna hiyo, Baba—kila mmoja. Pia naomba. . .nakuomba jambo hili, Baba, ya kwamba kila mtu aliye hapa asubuhi ya leo ambaye amenisikia nikisimulia ono hili, naomba kwamba nikutane na kila mmoja wao kwenye ng'ambo ya pili. Ingawa huenda ikawa kuna watu hapa ambao wanaweza kutokubaliana nami, na wanawake pia, bali Baba, usiache jambo hilo lituzuie. Naomba kwamba tuwakute kule watakapokimbia, pia, nasi tushikane sisi kwa sisi na kupiga kelele, "Ndugu yetu mpendwa." Jalia iwe kama ilivyoonyeshwa kule, Bwana, kwa kila mtu. Wote niliopata kuwapenda na wote waliopata kunipenda. Naomba ya kwamba itakuwa jinsi hiyo, Bwana. Nami nawapenda wote. Naomba waonekane, Baba. Nawapa Uzima wa Milele sasa. Jalia wao watekeleze sehemu yao kwa kuukubali. Kwa maana naomba katika Jina la Yesu. Amina.

Tuna muda mchache tu kuwaombea wagonjwa. Naona tuna msichana mgonjwa hapa na bibi fulani kwenye kiti. Naam, kwa ndugu zangu wa thamani sana, dada. Tafadhali msinielewe vibaya. Mi—mimi sijui yaliyotendeka. Sijui yaliyotendeka. Bali Mungu, wakati nitakapokufa, nijalie niende kule. Nijalie tu nirudi mahali pale, hapo ndipo ninapotaka kuwa, po pote pale. Mimi sijaribu kuwa Paulo aliyetwaliwa hata Mbingu ya Tatu. Sisemi hivyo. Ninaamini ya kwamba Yeye alikuwa tu anajaribu kunitia moyo, akijaribu kunipa kitu fulani kidogo kujaribu kunisukuma mbele katika huduma yangu inayokuja.

Hivi litaonekana jambo lisilofaa kama nikisoma kitu hapa kwa dakika moja? Itakuwa sawa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Moja la magazeti yanayoongoza nchini—Billy Graham: DK. BILLY GRAHAM ANAALIKWA KWA WAISLAMU. Ukurasa wa kwanza wa *Afrikaans Times*, tarehe 15, Februari, 1960. Mwandishi wa makala hii, aliyekuwa islamu

[Mwislamu] anafikiri ya kwamba ishara zinapaswa kufuatana na kuhubiriwa kwa Injili ya Kristo—yeye yule jana, leo na hata milele. Tunanukuu:

> Haya ndiyo Kristo aliyowaahidi, wafuasi Wake, aliposema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya; hata kubwa kuliko hizi atazifanya." Je! kanisa limewahi kufanya kazi ambazo. . .si—sifa za Kristo katika Biblia; linaweza leo? Je! kuna mtu mmoja wa walio mashuhuri sana wa kanisa anayeweza kufanya hata nusu ya miujiza iliyofanywa na Kristo? Hata bila kusema kazi kubwa zaidi. Je! wewe kama mtu binafsi anayejulikana sana, mwakilishi wa Ukristo unaweza kufufua. . .kuwafufua wafu waishi maisha ya kawaida? Unaweza kutembea juu ya bahari? Unaweza kuwaponya wagonjwa na kuyafungua macho ya vipofu? Si hii inalingana na kipindi kilichotajwa hapo juu kilichowekwa na Mwislamu, ama kilichowekwa. . .ama kanuni ya Kristo ambayo inafuata kama taarifa ya mahali fulani katika imani yako?

Mengi katika makala hayo ya Mwislamu huyo ni habari za uongo moja baada ya nyingine. Wao hawamsadiki huyu Mwislamu, lakini alisema kweli. Bali haya ndiyo waliyosema:

> Jibu zuri sana ni kusoma Biblia na kujua Kurani. Kurani inapungukiwa kwamba. . .inapungukiwa ukizilinganisha. Madai ya Uislamu ni makuu sana na yanashinda Ukristo, ni m-a-k-e-k-e matupu (nadhani ni makeke) ya kuwazia. Mwandishi hata hivyo aligusia jambo muhimu sana kuhusu miujiza kuwa mali ya kanisa. Lakini hapa tena tunatilia shaka uaminifu wa huyu mwandishi. Kwa maana ni nani angeonyesha ama kukanusha miujiza iliyofanywa na Kasisi William Branham mbele ya Waislamu katika Afrika Kusini, wakati elfu kumi walipolipokea, Kristo kama Mwokozi. Chini ya huduma ya William Branham huko Durban, Afrika Kusini na mahali pengine ulimwenguni kote, ama ya T.L. Osborn Afrika Mashariki. Bila shaka tunamuunga mkono Billy Graham asilimia mia moja. Tumezungumzia juu ya jambo linaloswaliwa. Hili jambo linaloswaliwa halina maana."

Bali kati ya kila kipengele chake, yeye aliniambia—kasema sisi ni washupavu wa dini; hatukujua tulilokuwa tunafanya. Iliwabidi kushuhudia katika gazeti lao wenyewe ya kwamba Mungu alitenda hayo hata hivyo. Mungu ni Mungu leo kama vile tu alivyowahi kuwa. Huenda usifikirie ya kwamba wao hawakuliamini; hawalioni. Halijafichwa; halifanyiwi pembeni. Mamia ya maelfu ya watu walioketi pale waliliangalia jambo hilo. Walipomwona yule mvulana kiwete aliyeteseka akija pale, na Roho Mtakatifu akamwambia juu ya maisha yake na kadhalika na kilichotendeka humo, na kuwaona Waislamu elfu

kumi wamejilaza chini kifudifudi, na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wao binafsi.

Tungali tuna akina T.L. Osborn, na kadhalika, ambao wangali wanawalisha kondoo chakula. Nakisia Ndugu Osborn hajashuka kwenda miongoni mwa Waislamu bado. Wao wanadai ya kwamba wana nguvu zaidi. Bali tungali tuna Mungu ambaye anaweza kuwaokoa kodoo kutoka kwa simba; anayeweza kuwaokoa kondoo kutoka kwa dubu. Na ilinifurahisha kujua ya kwamba itawabidi kuiandika na kuitambua. Wanafikiri hawaitambui. Wao wangeondoka na kuipa kisogo na kusema, "Loo, siku hizo zimepita." Waislamu wanasema, "Aha, wao, Biblia nzima imepita basi. Nyote mmekosea. Mnamwabudu mwanadamu. Mtu aliyekufa, na Jina Lake lilikuwa Yesu, Naye alikufa miaka mingi iliyopita, na hakuna kitu cha kama Yeye kufufuliwa." Bali hawangalisema hayo kwenye mkutano wa Durban.

Yeye alisimama pale akifanya mambo yale yale aliyofanya na kuwathibitishia. Sasa, hata madhehebu hayana budi kurudi . . . Mtu yeye yule aliyeniambia ingenibidi kuagiza mafundisho yangu juu ya Biblia yarudishwe ndiye iliyembidi kuandika hayo kwenye gazeti lao. Mungu atawafanya wamsifu Yeye hata hivyo. Hiyo ni kweli. Atawafanya wamsifu Yeye hata hivyo.

Nina msichana mdogo mgonjwa anayeketi hapa. Huyo ni mtoto wako? Ana shida gani, dada? Mama? [Yule dada anasema, "Kuvuja kwa damu kwenye ubongo."—Mh.] Kuvuja kwa damu kwenye ubongo. [Ndugu Branham anazungumza na mama wa mtoto anayeteseka—Mh.] Kuna jambo moja tu, Mama, anaweza basi . . . atamwokoa msichana huyo. Huyo ni Mungu. Mnajua hivyo. [Yule dada anasema, "Amekuwa afadhali sana kuliko alivyokuwa."—Mh.] Ninafurahi sana kwa jambo hilo. Umeshuka kwenda kule na kumwombea, Ndugu Neville? Tangu Ndugu Neville aliposhuka kwenda na kumwombea amepata nafuu kidogo. Tungali tuna wachungaji wanaojua chakula cha kondoo.

Una shida gani, dada mpendwa, unayeketi kwenye kile kiti pale? Wako? Kansa. Vema, kama nikiwauliza tu jambo fulani, labda papa hapa. Ni wangapi walio humu wamekwisha ponywa kwa . . . kansa, inueni mikono yenu. Angalia hapa, dada. [Yule dada anasema kitu fulani.—Mh.]

Mungu ndiye Mponya. Tunajua jambo hilo. Kama nilivyowaambia ya kwamba ningeshuka niende kule na kuondoa kule kuvuja kwa damu kutoka kwa yule msichana na kumpa afya, ningewaambia lisilo kweli. Ama ningeweza kuiondoa ile kansa kutoka kwa yule mwanamke. Bali najua kitu kimoja: kulikuwa na dubu, kansa, kivimbe, upofu, na hata mauti yaliyowashika ghafla baadhi ya kondoo wa Mungu siku moja. Nami nikatoka nikaenda kwa nguvu za Mungu, nikamuua na kumrudisha huyo kondoo. Hiyo ni kweli. Nasi tunaenda leo,

si na kitu kikuu fulani na fulani. Ninaenda zangu na kombeo tupu la maombi. Litamrudisha. Unaamini jambo hilo, sivyo, dada? Unaamini hilo, pia, sivyo, dada? Ni wangapi wenu sasa mnaamini kwa moyo wenu? Sasa, inamisheni vichwa vyenu ninapoomba. [Ndugu Branham anaondoka jukwaani kuwaombea wagonjwa—Mh.]

Waweza kuinua kichwa chako kwa dakika moja. Mchungaji ndiyo kwanza aniambie watu hawa walikuwa mahututi sana. Watapata afya. Ni sawa tu. Ahadi ya Mungu haishindwi. Tunaenda kuwaleta.

Wana ibada ya ubatizo. Kuna watu ambao hawana budi kwenda. Tutakuwa na ibada tena usiku wa leo. Kuna mtu hapa ambaye asingeweza kuja usiku wa leo na ungetaka tukuombee sasa?—ambaye hawezi kuwa hapa usiku wa leo. Waweza kuja hapa sasa hivi? Nyinyi ambao hamwezi kuja usiku wa leo—nitakuwa na wakati mwingi wa mstari wangu wa maombi usiku wa leo. Hawana budi kuwabatiza watu hawa. Una mvulana mdogo pale . . . Naam, ndugu, asante sana. Ni sawa kama nikiisoma baada ya muda kidogo ama sasa hivi . . . kama nikiisoma baada ya muda kidogo ama sasa hivi, . . . Asante, bwana.

Naam, kama mkitupa tu dakika moja ama mbili zaidi, tu- . . . halafu tutakuwa basi na ibada kwa ubatizo. Najua mtataka kuuona. Na wale wanaotaka ubatizo asubuhi ya leo, vema ninyi-—mabibi nendeni upande huu mkabadilishe mavazi yenu, na wanaume mwende upande huu. Halafu, wakati ninapowaombea wagonjwa, basi mtakuwa mkijitayarisha kwa ajili ya ibada ya ubatizo. Na wale sasa ambao . . .

Sasa, usiku wa leo nitajaribu kufanyiza mstari mdogo wa maombi usiku wa leo. Mara moja, mara watakapoingia. Nasi tutaanza katika Kitabu cha kwanza cha Waefeso usiku wa leo. Nasi tutakuwa na furaha sana sasa, kuwa pamoja nanyi humu. Kama hamna kanisa la kuhudhuria. Bali kama una mchungaji wako mwenyewe na kanisa la kuhudhuria basi wewe—wewe hudhuria kanisa lako la thamani mahali ambapo unapasidia. Kama ninyi, ambao itawabidi kuondoka, na mtaondoka wakati huu, Mungu awabariki. Mwe pamoja nasi tena mkiweza. Tutafurahi kuwa pamoja nanyi. [Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani—Mh.] Sasa wengine wenu mnapoviinamisha vichwa vyenu kwa dakika moja; tunataka kuomba.

Baba, ninakushukuru Wewe leo kwa ajili ya lile kombeo dogo la mchungaji, maombi yaliyomfanya simba kujisalimisha, na yule mwana-kondoo mdogo akatwaliwa ghafla kutoka kwake akarudishwa kwa mamaye na babaye. Namwombea ndugu yetu. Naomba ya kwamba utamleta salama pia, Bwana. Naomba kwamba ule msukumo wa damu na shida katika mwili wake

vikome. Naenda kumtafuta, Bwana, kumrudisha. Katika Jina la Yesu Kristo; na iwe hivyo. Amina. Mungu akubariki, ndugu.

Nikishuka kwenda kule namwona mvulana mwingine mdogo aliye kipofu. Ningetaka kusema jambo lingine moja. Nilikuwa mgonjwa sana...Nilikuwa ninatapika. Nami nikawaza...Sitaki ulikose hili kama ukiweza. Nikawaza, "Mungu, ningetoa nini kama ningalisikia mtu fulani akisimama nje."

Mke wangu angesema, "Billy, kuna mzee muungwana amekuja hapa kukuona." Na huyu hapa anakuja maskini jamaa mwenye kipara, huku masharubu yenye mvi yananing'inia usoni mwake.

Yeye angeingia na kusema, "Wewe ni Ndugu Branham?"

Ningesema, "Naam, bwana, ni mimi."

"Jina langu ni Simoni." Akanikumbatia kwa mkono na kuniangalia kidogo. Kasema, "Wewe ni mwamini, Ndugu Branham."

"Naam."

"Itakuwa sawa."—Simoni Petro wa Biblia. Jinsi ningalifurahia jambo hilo! Haingemlazimu kusema mengi—ni kunikumbatia tu. Ingekuwa sawa.

Halafu nini kilichonijia: Kwa msaada wa Mungu na kwa neema ya Mungu, kuna makumi elfu ya watu wangaliamini jambo lile lile kama ningaliwajia. Nami nikawaza, "Bwana, nijilie nimfikie kila niwezaye, basi. Nije tu." Nilifikiri kama Simoni angeninino tu...Paulo—baadhi yao waingie, waseme, "Wewe ni Ndugu Branham?"

"Naam."

Waweke mikono yao juu yangu na kuniangalia na kusema, "Vema, Ndugu Branham"—watoke tu. Ningepata afya. Ningekuwa mzima. Bila shaka. Nikasema... "Jamani, ujasiri wangu ungeingia papo hapo." Ningesema, "Nitapata afya." Naam, bwana. Na kuna watu wanaoamini jambo lilo hilo leo. Na hilo ndilo ninaloshuka kuja hapa kufanya: kuwawekea nyinyi mikono, na kumwomba Mungu. [Ndugu Branham anaendelea kuwaombea wagonjwa.—Mh.]

*Mfalme Aliyekataliwa* SWA60-0515M
(The Rejected King)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 15 Mei, 1960 katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1992 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org